



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Ishirini – Tarehe 25 Mei, 2022

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. MASWALI:

Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

104. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

Dunia imekumbwa na janga la mabadiliko ya tabianchi ambapo Zanzibar kama sehemu ya dunia pia imeathirika na tatizo hilo.

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyanusuru maeneo yaliyoathirika na tatizo hilo.
- (b) Kwa kuwa upandaji wa miti ni moja kati ya udhibiti wa janga hilo. Je, Wizara yako inashirikianaje na wananchi katika kuwashajihisha na kuwawezesha katika upandaji wa miti.

Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi wa Uwekezaji:

184. MHESHIMIWA SHADYA MOHAMED SULEIMAN (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Hivi sasa kumekuwa na ongezeko kubwa la watu wanaojifanya maafisa kutoka Wizara ya Uwekezaji na kuwapigia simu wananchi kuhusiana na mikopo.

- (a) Je, Wizara inalifuatilia vipi suala la mikopo ambayo inatarajiwa kutolewa ili kuepuka wananchi kutapeliwa.
- (b) Je, Wizara imeshatoa elimu kiasi gani juu ya dhana nzima ya mikopo hii.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

122. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ni uamuzi sahihi uliofanywa na Serikali tokea mwezi Septemba 2021 wa kuziua meli tatu ili kutoendelea kuingiza hasara ya kuzitunza kwa Serikali.

- (a) Je, ni kwa nini hadi sasa Serikali haijazuiza meli hizo.
- (b) Je, ni kwa bei na utaratibu gani bora na sahihi Serikali imekusudia kuutumia katika kuziua meli hizo.
- (c) Je, Serikali imetumia wataalamu na washauri gani na kwa gharama gani katika kupata suluhisho la meli hizo.

123. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na malalamiko mengi na yaliyohibitika kutoka kwa wafanyabiashara kuhusu kupanda kwa gharama za kuleta na kutoa mizigo katika Bandari ya Zanzibar ambazo, kwa kiasi kikubwa, zinasababishwa na muda wa kusubiri (waiting time) kwa meli za mizigo zinazolingia Zanzibar. Pamoja na kwamba tatizo hili lilirithiwa na Serikali ya awamu ya nane kutoka Serikali ya awamu ya saba na kwa kuwa jambo hili limekuwa likiongeza gharama za maisha moja kwa moja kwa wananchi, ni dhahiri kwamba ahadi na mipango ya awali ya Serikali ya awamu ya nane inaonyesha imefeli:

- (a) Je, kwa wastani, kati ya mwezi Januari na Aprili 2022 ni upi umekuwa muda wa kusubiri (waiting time) kwa meli za mizigo zilizoingia kupitia Bandari ya Zanzibar.
- (b) Je, ni kiasi gani cha fedha kinachotakiwa kulipwa na meli kwa kila siku ya kusubiri.

- (c) Je, ni upi mpango wa dharura na mpango wa kudumu wa kupunguza muda wa kusubiri kwa meli za mizigo zinazoingia Bandari ya Zanzibar.

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

131. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Hatua zilizochukuliwa na Serikali ya awamu ya nane katika mchakato wa uchimbaji wa mafuta Zanzibar ni wa kupongezwa. Hata hivyo, taarifa kuhusu mpango huo zimekuwa zikififia na wananchi wanalalamika kukosa taarifa zilizo kamili na kuwepo kwa ukimya usio wa kawaida.

- (a) Je, ni kwa nini Serikali imekaa kimya kwa muda mrefu kuhusu mpango wa uchimbaji mafuta Zanzibar.
- (b) Je, hatua ipi inaendelea na ipi imekamilika katika mchakato wa kuchimba mafuta ndani ya Zanzibar.
- (c) Je, ni lini Zanzibar itaanza kuchimba mafuta na kwa utaratibu upi.

II. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
25 Mei, 2022.


(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA